



Shasta

Kuwa mjanja, **Jikinge!**

Katibiwe
huo
ugonjwa wa
ngono!



Tambua ukweli
juu ya magonjwa
ya ngono.



Ni yapi hayo?

Kama utakuwa na ugonjwa wa ngono, hii hukuongezea wewe uwezekano wa kuambukizwa VVU kutoka kwa mtu aliyeambukizwa. Hii ni kwa sababu magonjwa ya ngono husabaisha vidonda na majeraha ambayo hurahisisha upenyaji wa VVU.

Unawezaje kutambua kuwa una maambukizo ya magonjwa ya ngono?

Si magonjwa yote ya ngono yatakuwa na dalili zinazofanana. Zifuatazo ni baadhi ya dalili zilizozeleka.

Mgonjwa ya ngono yaliyozoeleka ni kama yafuatayo

Malengelenge


Kaswende

Clamidia

Kisonono

DALILI

- Muwasho wa moto ndani na nje ya uke
- Kutokwa damu wakati si siku za hedhi
- Maumivu ukeni wakati wa kujamiiana au kutoka damu baada ya kujamiiana
- Vidonda, sundosundo na malengelenge kuzunguka mdomo, uke au njia ya haja kubwa
- Maumivu kwenye viungo yanayoambatana na homa
- Mwasho wenye maumivu makali wakati wa haja ndogo
- Kubadilika kwa rangi, harufu au kiasi cha maji maji ya ukeni
- Kusikia maumivu wakati wa kutoa haja ndogo au kubwa
- Kutaka kwenda haja ndogo mara kwa mara
- Maumivu chini ya kitovu



***Ajabu; Mwanamke
anaweza kuwa
ameathirika na
magonjwa ya
ngono kwa muda
mrefu bila kujihisi
wala kuonyesha
dalili yoyote***

Hivyo kama ulifanya ngono bila kinga usisubiri mpaka kuona dalili ndiyo uende kutibiwa. Chukua hatua sasa!

Ukijihisi una ugonjwa wa ngono ufanye nini?

- * Usingoje kuwa dalili hizo zitaondoka - *hazitaondoka*
- * Magonjwa mengi ya ngono yanatibika kirahisi. Kama unahisi una ugonjwa wowote au dalili zilizotajwa hapo juu wahi hospitali .
- * Kumbuka kadiri unavyopata matibabu mapema ndivyo inavyokuwa rahisi kutibika.

Nini kitatokea kama hutapata matibabu?

Magonjwa ya ngono yasipotibiwa mapema, yanaweza kuleta madhara ya kudumu kama ugumba kwa wanawake. Kumbuka ugumba hautibiki.

Unafahamu namna ya kuhakikisha huambukizwi tena?




Matumizi ya kondom yaliyo sahihi na ya mara kwa mara ndiyo njia bora zaidi ya kukuinga na magonjwa ya ngono.

Kondomu zinapatiana kwa urahisi katika maduka yaliyo karibu na wewe kama kioski, duka la dawa, supamaketi, kwa mangi nk

Unaweza kupata kondom kwa bei rahisi kwa kiasi cha Tshs 200 kwa pakiti yenye kondom 3

Tumia komdom kila mara unapofanya ngono ili kujilinda na mganjwa yatokanayo na ngono pamoja na VVU/UKIMWI



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

